KITABU KIDOGO CHA EPWORTH

MWONGOZO WA KULIANZISHA NA KULIKUZA KUNDI

Toleo la 1;1

Kimetayarishwa na ofisi ya makao makuu ya kundi la Epworth
January 26,2011

PATANO LA KUNDI LA KANISA LA EPWORTH

Sisi tulio washirika wa ----------Kanisa ,kwa siku hii ya leo ----------
tunakubali kulitegemeza na kulisaidia kulianzisha kundi la mahali la kundi la Epworth.
Tutafanya kuliwezesha na kuitia moyo huduma hii ya vijana.

---------- ----------

Mchungaji Tarehe

---------- ----------

Mwenyekiti wa baraza auKiongozi wa mlei Tarehe

AHADI YA KUNDI LA EPWORTH

Kwa juhudi nitajitafutia mwenyewe nikisaidiwa na mungu pamoja na ule wa dada na kakazangu ,na kufanya kila ninaloweza kuwasaidia wengine waweze kupata maisha ya juu zaidi yanayofanana na maisha yake yesu.Nitajitahidi niwezavyo kuziacha aina zote za matendo na tabia yanayokuwa kinyume na mafundisho ya yesu kristo, na nitahudhuria kwenye mikutano ya kundi la Epworth na ya kanisa, na kuweza kuwa msaada kwa hayo.

---------- ----------

Imetiwa saini na kiongozi wa kundi la Epworth tarehe

…….

Andika jina kamili

Kanisa la kundi la ufadhili la Epworth na mahali lilipo.

Kitabu cha kiongozi wa epworth v,1.1

Jumuiya ya vijana wa kimethodisti

January, 26/2011

Kitabu cha viongozi wa vijana

Ofisi kuu ya “epworth:”

W1008 froelich rd –sollivan,wi

u,s,a

Mkurugenzi ; ken rheingans
Simu 414-807-3193

Barua pepe ; reheingans@ao1.com
www.epworthleague.Org

copyright 2011 Pleasant Valley United Methodist Church

Yaliyomo;

Wadawa wa kitabu hiki ……..……
Kazi ya kundi la Epworth……
Mwanzo wa Epworth…….
Makundi ya Epworth…….…….
Uanachama…….
Kikomo cha umri……
Ukiri wa imani ya Epworth……
Ofisi kuu ya kundi la Epworth……
Msaada wa namna ya kulianzisha kundi……
Tovuti ya kundi la Epworth ……**.....**
Sera za kundi la Epworth……
Sera za kundi la Epworth –Mikutano……..
Mafunzo ya kiongozi wa kundi la Epworth…….
Mafunzo ya kiongozi wa kundi kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo……
Mpango wa ajira wa kundi la Epworth ……
Mpango wa kusaidia malezi wa Epworth…….
Mpango wa Epworth wa Huduma magereza……
Washauri wa viongozi wa makundi…….
Kulianzisha kundi…….
Hatua ya 1; Wasiliana na ofisi kuu ya Epworth kwa ushauri wa awali……..
Hatua ya 2; Fanya mkutano pamoja na watu wenye nia ya kulianzisha kundi…….
Hatua ya 3 ;Fanya mjadala wa awali pamoja na mchungaji wa kanisa lenye ufadhili…….
Hatua ya 4; Amua ni viongozi wapi watakaokuwa wanalianzisha kundi……..
Hatua ya 5; Ahadi zilizosainiwa kwenye Ofisi kuu ya Epworth……
Hatua ya 6; Kutakuwa na baraza la uongozi la kanisa lenye kufadhili……..
Hatua ya 7;Fanya mkutano wa kulianzisha kundi…….

Taaarifa ya mawasiliano

Ofisi kuu ya Epworth

Mkurugenzi – Ken Rheingans

414-807-3193

Barua pepe kwa Rheigans@ao1.com

Huduma za kulianzisha kundi –Sue Rheigans (suerheingans @ao1.com)

JiLLmkahn@q mail.com)

Mratibu wa Volunteer-Bill Lurvey(w/urvey@charter;net)

Mkurugenzi wa kujenga jamii—Anne Gibsonfumc@yahoo.com)

Mkurugenzi wa umisheni-Samantha Ruchl(samala 3321@ gmail.com)

Mkurugenzi wa ukuzi wa kiroho – Owen Cooper (Owen cooper22@gmail.com)

Mhariri wa gazeti la Epworth Nerald –Adam Rheingans2ao1.com

Wengi wa wanachama wengi wa ofisi kuu waweza kupatikana kwenye “Face book”

Barua pepe:

Ofisi kuu ya kundi la Epworth

W1008 Froelich Road

Sullivan, W1 53178

U.S.A

Walengwa wa kitabu hiki .
Makusudi ya kitabu hiki ni kutoa namna gani, na taarifa ya nyongeza kwa mtu yeyote anayeanza ,au kujiandaa vipya ,na pengine kuwa na mpango wa kulianzisha kundi la

vijana wa United Methodist katika namna ya mtazamo wa Epworth.Wale wanaojihusisha na huduma ya vijana watagundua kuwa mambo yaliyomo ni ya muhimu vilevile.

Mtazamo wa kundi la Epworth .

Kundi la Epworth ni jipya kwa ulimwengu wote, Jumuiya ya vijana wa United Methodist ni wale wanaokuwa na umri kutoka miaka 18-35. Jumuiya imekuwa na sura ya kanisa la mahali ulimwenguni pote. Ofisi kuu ya Epworth ndiyo inayo wapatia msaada.

Dhamira ya kundi la Epworth

Katika kuwatia moyo vijana na kuwafanya wawe na tabia ya kumtegemea Yesu Kristo ulimwenguni pote kwa njia ya kuijenga jamii kuwa na moyo wa umisheni pamoja na kukua kiroho.

Mwanzo wa kundi la Epworth

Jina la kundi la Epworth linatokana na mji wa Epworth ,huko uingereza,mahali alipozaliwa John Charles Wesley ambao walikuwa wamealianzisha kanisa la Methodist.
Kwa nyongeza zaidi,jina la kundi la Epworth lilitumika tangu mwaka 1889 mpaka 1939 kama ni jina la jumuiya ya vijana wa kanisa la Methodist.Miaka mia moja iliyopita kundi la Epworth lilikuwa na maelfu ya vijana ulimwenguni pote.Yapo mambo mengi tungeweza kujifunza kutokana na kundi hili la kwanza hata baadhi ya mipango yake tuanaitumia mpaka leo.

"Mungu anaendelea kuziandaa nguvu zaidi kwaajili ya kusonga mbele hatimaye tufikie kushinda ulimwengu."Miongoni mwa nguvu hizi amewafanya watumishi wake walianzishe kundi la Epworth.Unatakiwa ushiriki katika kundi hili bila shaka kwa maombi yako,mivuto uliyonayo,fedha itakuwa ya thamani pia,lakini umuhimu wa wajibu wako na hesabu yako itategemea ni nini ulichokitenda.
"Kundi la Epworth lina nafasi yake katika umethodist"(Nukuu ya Mchg.J.B.Robenson 1890)

Mpango wa kundi la Epworth unampatia fursa kila mshirika "kwa kila mtu kazi yake".Kunaweza kuwapo na nafasi maalumu kwa kila mtu,na wajibu ambao unaeleweka kwa urahisi,na pamoja na huduma halisi pamoja na ukuzi wa mtu binafsi ambao unapatikana katika kila wajibu(Nukuu: Dan Brearley Brummit1914).

Kwa msaada wake Mungu tunatumaini kuuwasha moto ule wa kundi la kwanza la Epworth kwa ajili ya kutoa huduma na kuwawezesha vijana kwa njia ya kanisa la United Methodist ulimwenguni pote.

Maeneo ya kundi la Epworth ;
Maeneo ya kundi la Epworth ni maeneo yale ambayo kazi ya Epworth inafanyika. Pia sehemu ile ambayo vijana wanaweza kutafuta njia ya kuwa kundi na kuwepo katika kukua na kutembea na yesu kristo.

Ni vigumu kuwa na kundi lenye mafanikio—kwa kuifungua milango yenu na kuzituma kadi za posta peke yake haitoshi. Kundi lenye kufanikiwa ni lile ambalo litajiweka mahali pa kuhitajika na jamii ile inayoihudumia.

Makundi kwa kawaida yanafadhiliwa na kanisa la United Methodist na kushirikiana kwa mtindo wa kawaida wa uendeshaji ambao daima unalenga kwenye kiwango chenye maeneo matatu ya msingi.

- Ukuaji wa kiroho.
- Umisheni
- Kuiendeleza jamii.

Kundi la Epworth,ni kama baiskeli au ndege ulaya.
Katika kutaka kudumu lazima iendelee na mwendo.Haipaswi kubaki imesimama tu na haiwezi kubaki imesimama tu na ikaleta mafanikio.

Vijana wanapenda kushughulika na wanapenda kufanya shughuli. Hawatabaki sehemu ile ambayo haina shughuli.Lakini pia wanaomba shughuli yenye maana.Wanapaswa kuwa na shughuli yao yenye utendaji.Hawajali kucheza kwenye huduma ya kikristo,kupiga porojo bila kukoma juu ya huduma hiyo pasipo kufanya chochote.

Dan Brearley Brummitt 1914.

UANACHAMA

Milango ya kuingia katika kundi la Epworth ipo wazi kwa wote. Hakuna masharti ya uanachama isipokuwa kwa viongozi moja wapo,wanaoshiriki si lazima wawe washiriki wa kanisa la United Methodist, hata hivyo imesisitizwa.

Umri unaotakiwa;

Umri wa chini ni miaka 18 na umri usiozidi miaka 35.Mara nyingine hasa kundi linapoanza baadhi ya vijana zaidi ya hapo wanaweza kuhitajika.

UKIRI WA KUNDI LA EPWORTH

Nitajitahidi mwenyewe nikiwa na msaada wa Mungu na ule wa ndugu na dada zangu,na kufanya yale niwezayo katika kuwasaidia wengine waweze kukifikia kiwango cha juu cha maisha yenye kufanana na yesu. Nitajitahidi sana kuyaacha matendo na tabia yote yaliyo kinyume na mafundisho ya Yesu Kristo,na nitahudhuria mikutano yote ya kundi la Epworth na ya kanisa na kuwa na nafasi ya kuiwezesha.

Tamko la imani ya Epworth

Kundi la Epworth linaifuata imani ya kanisa la United Methodist. Kwa taarifa zaidi, tafadhali uende kwenye tuvuti uangalie kwenye http;//archives.
Umc,org/interior,asp,mid=519

OFISI KUU YA KUNDI LA EPWORTH

Ofisi kuu hutoa huduma muhimu zifuatazo

1) Kusaidia kulianzisha kundi.
2) Kuiendesha tuvuti ya Epworth

3) Kazi za kundi la Epworth kwa mafunzo
4) Waangalizi wa viongozi wa makundi kila mojawapo inatolewa maelezo zaidi hapo mahali

MSAADA KWA AJILI YA KULIANZISHA KUNDI

Kimsingi ofisi kuu inalenga juu ya kuwasaidia watu binafsi namna ya kuyaanzisha makundi .Wale wanaojitolea kwenye ofisi kuu watakusaidia hatua kwa hatua katika kulianzisha kundi. Orodha ya hatua hizo zaweza kupatikana baadaye katika kitabu hiki;
(Wasiliana na ofisi kuu Tazama nyuma ya kitabu hiki)ikiwa wakati wowote ukiwa na maswali au ukimtaka mtu wa kuzungumza naye juu ya mawazo au mambo uliyonayo.

Tovuti ya Timu ya Epworth

Hivi sasa zipo tuvuti mbili ambazo ofisi kuu inazozitumia . www.epworth league.org 356243866782

Hii ni tuvuti kubwa ya kundi la Epworth.Kwa sasa ni tuvuti ya kawaida sana iliyo na taarifa muhimu ikiwa na mahali unaweza kulipata toleo la siku hizi la maandishi haya .Tuvuti inayo kalenda ya matukio ya msingi ya kundi la Epworth kama vile safari za kimisheni,mazoezi na shughuli za Epworth.Hapo baadaye hii tuvuti itahusisha ushirikiano na utendaji wa kazi uliobuniwa ili kuwasaidia watu binafsi katika kuyaanzisha na kuyakuza makundi.Kutakuwa na hiari kwa makundi ya vijana wa United Methodist ya kujisajili kwa tuvuti ya makundi ya Epworth.Yatahitaji kuijaza fomu ya maombi na kutia sahihi kwenye hati ya agano ambayo itasainiwa na viongozi wa makundi ya vijana .Tunategemea kuwa hii tuvuti kuja kuwa ndicho chombo cha msingi cha timu ya Epworth kwa kuyaruhusu makundi na watu binafsi katika kubadilishana uzoefu,matatizo na Baraka kwa manufaa ya watu wengine.

Pia kundi la Epworth lina kundi la :Tazama Kitabu”Ni mahali pazuri pakukutana na wengine wanaoipenda timu ya Epworth.
www.Face book com/group php r gid =356243866782

Taasisi ya kundi la Epworth

Taasisi ya kundi la Epworth ni ofisi kuu ya mipango inayotoa mafunzo na nafasi za masomo kwa ajili ya vijana.Kwa sasa hivi inazo;

- Kusanyiko la kazi za Timu ya Epworth.
- Chuo ambacho kinatoa mafunzo juu ya uongozi.
- Mpango wa ajira ambao makundi yanaweza kuzipatia jamii zake.
- Mpango wa huduma ya magereza.

Endapo utapenda kusaidia kuikuza mipango na kutoa vifaa vya kufundishia kwa ajili ya shule ya timu ya Epworth tafadhali wasiliana na ofisi kuu(Angalia nyuma ya kitabu hiki)

Mikutano ya kazi za Timu ya Epworth .

Mikutano ya kazi za timu ya Epworth ni ya aina yake yenye kueleweka kama ni ;vyuo vya Timu ya Epworth ;Ni yenye gharama ya chini ambayo inawezeshwa na ofisi kuu na kundi moja na hufanyika karibu na makundi yanayoiwezesha. Mikutano yaweza kuchukua kuanzia siku moja au saba.

Karibu ya kazi za Timu ya Epworth itakuwa na uwakilishi wa kisa kimoja au zaidi wa visa vifuatavyo;

- Ukuzi wa kiroho
- Kuijenga jamii
- Umisheni
- Mipango ya kulea watoto.

Mipango ya Timu ya Epworth ya huduma ya magereza

Vilevile tunatafiti juu ya kuwa wawezeshaji wa kutunza kumbukumbu za kazi za makundi ya Epworth.Haya mambo yatafanyika kwenye tuvuti na kuwashawishi watu juu ya yale wanayo yafanya na kuhamasisha kidiplomasia.

Kufanya mikutano kwa video na kutoa mafunzo kwa njia ya tekinolojia ya tuvuti ili kufanya watu washiriki kutoka nyumbani au kanisani kwao.

Endapo kundi lako lingependa kuzisaidia shughuli za Epworth katika jamii yako tafadhali wasiliana na ofisi kuu.

Mafunzo ya kiongozi wa kundi kwa ajili ya wanafunzi wa chuo.

Kazi ya kundi la Epworth kwa sasa inao ubia na chama cha washona hema ``` ili kuukuza mpango wa kufundisha juu ya uongozi ili kuwasaidia wanafunzi waliotangulia vyuoni namna ya kulianzisha kundi la Epworth baada ya kuhitimu.

Mafunzo yatatolewa kwa wanafunzi walioingia mapema chuoni hapohapo pamoja na mipango ya huduma ya United Methodist na itayahusisha mambo yafuatayo;

- Washa mbili hadi tatu ambazo zote kwa pamoja zitachukua muda wa karibu ya masaa mawili.
- Kwa kuunganika na mshauri aliyejitoa na mzoefu wa kundi la Epworth.
- Siku sita za kufundisha juu ya uongozi wakati wa likizo ya chuo wakati wa baridi.
- Kutoa msaada wa kuliunganisha na kanisa lenye kutoa ufadhili.

Mpango wa ajira kundi la Epworth

Mpango wa ajira ni wa mtazamo tofauti tofauti .

Yaani unafanywa na kuendelezwa na kundi la huduma ya Epworth kusudi lake ni kuwasaidia vijana wapate ajira au hata kupata kazi bora zaidi.Hii imekusudiwa ifanywe na kundi la mahali likisaidiana na kundi linalotoka kwenye kundi la kanisa linalotoa ufadhili.Washiriki wakongwe wakanisa watapewa fursa ya kueleza juu ya fani zao za kazi wanazozitafuta pamoja na kazi zinazoweza kupatikana katika jamii kwa ajili ya vijana

Huduma itahusisha msaada wa kupata kujenga tena kutafuta kazi,kutoa usaili,kukuza mbinu za mawasiliano kati ya mtu na mtu ,mpangilio wa kazi.

Mpango huu hautoi nafasi muhimu kwa kundi la mahali tu bali pia ni wapekee wa kuwaendea wale ambao pengine hawataweza kujiunga na kundi.

kundi la Epworth -mpango wa ajira .

Maelezo zaidi ya mpango huu yanapanuliwa na yatapaswa yawe tayari ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2011. Makundi yanayo karibishwa kuanza utendaji juu ya mpango huu kabla ya maelezo ya kina hayaja chapishwa na makao makuu.Kama kundi lenu linaanza juu ya hiki kitabu,tafadhari utupe taarifa jinsi gani mambo yanavyoendelea ili kwamba wengine waweze kunufaika na uzoefu wenu.

Mpango wa Epworth wa kusaidia kulea

Mpango wa kusaidia kulea ni mpango mwingine tena wenye mtazamo tofauti pia unaendelezwa na kazi za timu ya Epworth.Lengo la mpango huu ni kuwasaidia wazazi walio vijana kwa kiwango cha maswali yanayo husiana na malezi ,mafundisho na mahitaji. Pia umekusudiwa kuendeshwa na kundi la mahalilikishirikiana na kundi la kutoka kanisa linaloleta ufadhili.Washiriki wakongwe wa kundi watapewa nafasi ya kushuhudia juu ya malezi yao na vijana.

Kama vile mpango ule wa ajira ,mpango huu unalipatia kundi nafasi ya kutoa huduma muhimu kwa jamii ya mahali ,lakini pia ni mpango wa pekee kwa ajili ya kuwafikia wale ambao wanaweza kukosa kujiunga na kundi.

Mpango maalumu ungali unaandaliwa lakini unatazamia uwe na mambo yafuatayo;

- Kuzitambua huduma za jamii zinazoweza kuwapo kwa wazazi .
- Kuyatambua matakwa ya matunzo ya mtoto.
- Kuunganishwa na wazazi wengine walio vijana
- Madarasa ya namna gani ya kuwaleta watoto
- Namna yakutafuta mambo muhimu ya kuwalelea .
- Mpangilio wa gharama ya chini ya familia kwenda nje kwa matembezi (outings)(.kufungamanisha na timu ya kuijenga jamii) .
- Mpangilio kamili wa matembezi ya kielimu kwa ajili yawatoto waliosoma shule nyumbani.
- Kuunganishwa na wazazi wakongwe na mababu ambao wanaweza kuwa washaurri wa wazazi vijana.
- Kuyatoa mawasiliano ya moja kwa moja ya simu ambako waweza kupata msaada wa tatizo lako.

Maelezo ya kina juu ya mpango huu utapatikana kutoka kazi za Timu ya Epworth ndani ya robo ya mwaka 2011.

Makundi yanakaribishwa kuanza kuutendea kazi kabla ya maelezo ya kina hayajachapishwa na ofisi kuu.Ikiwa kundi lako linaanza na mpango huu,tafadhari utujulishe namna gani mambo yanavyoendelea ili kwamba watu wengine wapate kujifunza kutoka kwako.

Huduma ya Epworth kwa magereza .

Mpango huu utatoa maelekezo namna ya kuanza kutoa huduma magereza.Maelezo kamili yatapatikana baadayemnamo mwa 2011.

Washauri wa viongozi wa makundi.

Washauri wa Timu ya Epworth watakuwa ni chombo cha msingi wa kuyaanzisha na kuyakuuza makundi ya Epworth.
Washauri wa Timu ya Epworth ni watu binafsi ,wenye kuipenda huduma ya vijana ndani ya kanisa la United Methodist kwa nyongeza ,
Washauri wa Timu ya Epworth wanauzoefu wa moja kwa moja na huduma ya vijana na utendaji wa kanisa la United Methodist Church;Watatia moyo watatoa mwongozo na ushauri kwa viongozi wapya wa makundi.
Kama unayonia ya kumpata mshauri akusaidie wewe na kundi lako ,wasiliana na ofisi kuu .

Kulianzisha kundi;
Katika kulianzisha kundi la Epworth ni rahisi sana kuanza endapo unao viongozi na wenye kupenda na kulipata kanisa lenye kukuwezesha.Hatua zake zimeorodheswa hapo chini .Kama kwa saa yoyote unalo swali au hitaji,wasiliana na huduma za kulianzisha na ofisi kuu(Angalia nyuma ya kitabu hiki kwa taarifa zaidi).

Hatua ya kwanza (1)
Kulianzisha kundi la Epworth
Wasiliana na ofisi kuu ,taarifa ya mawasiliano yaweza kupatikana nyuma ya kitabu hiki.Watakujibu swali lolote ulilonalo na watakusaidia na hatua zinazofuatia .Pia watakuthibitishia kwamba umeipata taarifa ya hivi karibuni na wanaweza kukuunganisha na wengine katika eneo lako kwa wale wanao husika na timu ya Epworth.Hii itatusaidia sisi kukuunganisha na wengine wanaolitafuta kundi katika sehemu uliyopo.

Hatua ya pili(2)
Fanya mkutano pamoja na watu wenye nia ya kulianzisha kundi.

Unaweza kutaka kufanya hili kwenye eneo la wazi ambalo limezoeleka kama vile kwenye mgahawa,au hotelini washirikishe Epworth inahusika na nini.
Kukutana na mchungaji wa kanisa linalokupatia ufadhili na umpe huyo mchungaji kitabu cha maelezo ya kundi la Epworth.
Wajibu wa kanisa linalofadhili (sehemu ya A ya mwisho wa kitabu)pamoja na nakala ya ahadi ya kundi la Epworth. Maandiko yote yanapatikana kwenye tuvuti.

Kwa busara na kwa nafasi timu inakuja kwa msaada wa mchungaji .Ameubeba mzigo ambao timu haiwezi kumpunguzia .Kila sehemu yake ---------- idara inahisi baadhi ya maeneo ni ya uangalizi na mzigo wa mchungaji.Amewekwa kuwa wakili wa kampuni ya watenda kazi wenzake na zaidi kwa kuiongeza mamlaka yake katika kutumika zaidi ---------- .
Kundi linamwandalia njia mchungaji;
Hii inaonekana ni kweli na watu wa nje na watafutaji .

Kundi laweza kuwafikia kwa urahisi na haraka kuliko mchungaji.
:Timu ya Epworth , nafasi yake ndani ya Umethodist :
Na Mch.J.B.Robenson,1890

Hatua ya 4
Amua ni nani watakao kuwa viongozi wa asisi.
Kiwango cha chini viongozi watatu wanaweza kulianzisha kundi ,Mmoja wao shart awe mshiriki wa kansisa la United Methodist ingawaje si lazima kwa kanisa linalowezesha kundi .

Makundi kwa kila moja litakuwa na viongozi sita na kila mmoja akishika wajibu ufuatao;
1.Rais
2.Kiongozi wa ukuzi wa kiroho
3.Kiongozi wa timu ya umisheni
4.Kiongozi wa kuijenga jamii
5.Mtunza hazina.
6.Katibu.

Hata hivyo ikiwa viongozi wapo chini ya watu sita ,kila nafasi lazima ijazwe na kwa hakika mtu mmoja hawezi kuwa na timu zaidi ya moja .
(Ukuzi wa kiroho , umisheni kuiendeleza jamii)wajibu wa kiongozi.kwa nyongeza mchungaji mfadhili kiongozi mlei, au kiongozi mwingine wa kanisa katika wajibu wa kutopiga kura ,aweze kufahamika.

Endapo viongozi watatu hawapo,watu wengine wanatiwa moyo waweze kushirikiana na kundi jingine hadi watakapopatikana idadi ya viongozi wanaopaswa kuwapo.kama hakuna makundi yaliyo karibu unaweza kujisajili na ofisi kuu ya Epworth kama ;kundi linaloanza ; ambalo baadaye tutalifafanua vema chini ya ;kundi la muda ;kundi la muda linaainishiwa juu ya wajibu wake na linaweza kuelekezwa karama zinazotolewa na watu binafsi na kutoa huduma nzuri na nafasi ya ukuzi wa mtu binafsi kwa kila mmoja.Makundi binafsi yatalenga hasa juu ya baadhi ya timu kuliko zingine.Ingawaje makundi yote ni lazima yajaribu kufikia kiwango cha kutoa msaada kwa kila timu.kwa nyongeza viongozi wote wa kundi wanatakiwa kuweka sahihi zao kwenye mkataba wa Epworth ingawa hawatakiwi wafanye hivyo.

Hatua ya 5-Barua pepe za mkataba wa Epworth zilizotiwa sahihi ya makao makuu.

Angalia nyuma ya kitabu kwa ajili ya mawasiliano .kwa kadri unavyowapata viongozi zaidi endelea kuituma mikataba walioitia sahihi zao.Itakuwa muhimu kuionyesha mikataba hiyo kila mara.kwa sasa hivi inatakiwa ipelekwe mara moja kwa mwaka.

Hatua ya 6;Kutana na baraza la uongozi la kanisa linalotoa ufadhili mara moja kwa mwaka.

Makanisa yote ya United Methodist yanatakiwa yawe na baraza la uongozi , na hasa likijulikana kama ni ‘Ad Council: kundi hili kwa kawaida hukutana baada ya robo mwaka au kila mwezi kwa hiyo utataka uipate kalenda yao mapema iwezekanavyo.

Mchungaji wako ameanza kukusaidia juu ya hili utatakiwa uzilete nakala za kitabu cha matangazo ya timu ya Epworth; kazi ya kanisa linalotoa ufadhili ‘barua na mkataba wa kanisa wa timu ya Epworth .waweza kupatikana nyuma ya kitabu hiki.Mpaka hapa utakuwa tayari umevitoa vyote hivi kwa mchungaji ili kwamba hakuna cha kushangaza mkutanoni.

Bila shaka kwenye mkutano wako wa kwanza kutakuwapo na kura ili kuliwezesha kundi lako na utazipata sahihi mbalimbali hapohapo.Nyaraka ya mkataba uliosainiwa waweza kutumwa au kuchapwa au kutumwa kwa timu ya Epworth makao makuu.Angalia nyuma ya kitabu hiki ,hii pia ni nafasi nzuri kwako kuituma **;**fomu ya usajili wa Epworth’ inayopatikana kwenye sehemu ya nyongeza B , (kiambatanisho B)

Ikiwa ni kwa sababu fulani kanisa likijisikia haliwezi kuliwezesha kundi lako au kutia sahihi kwenye mapatano ,tafadhali wasiliana na mshauri haraka iwezekanavyo.Anaweza akakusaidia katika hili kwa sababu yawezekana katika hali hiyo akakosa uthibitisho.ofisi ya makao makuu itakuwa tayari kuwasaidia kulitafuta kanisa linginela kuwawezesha.

Hatua ya 7;
Uwe na mikutano ya maandalizi ya kuanzisha

Sasa unahitaji kuwa na mikutano ya awali/ utapaswa kupanga mikutano michache ya maombi.unaweza kuifanya mikutano michache ya awali ikawa husisha viongozi peke yake.Usiweke akilini kwamba endapo utaanza na kundi dogo sana na linawafikia watu wengi ambao hawajafahamika na kanisa waweza kuanza mikutano ya mipango na matukio ya ushirikiano hata kabla ya kuanza na mikutano ya maombi.

Hatua ya 8;

Gharama ya nafuu ya kundi lako linagharimu muda wa juhudi ;Waweza kuyabandika matangazo kwenya mbao za matangazo mbalimbali na kanisani kwako.Endapo utakuwa na vifaa vya matangazo vyenye kuleta ufanisi tafadhali ishirikishe ofisi kuu pengine watakutumia vifaa hivyo kwenye tuvuti;

AINA YA KUNDI

Makundi yote ya Timu ya Epworth yanayo miundo mitatu yenye kulenga maeneo haya;

- Ukuzi wa kiroho
- Umisheni
- Kuijenga jamii

Tangu mwanzo wa kulianzisha kundi ,waasisi ni lazima wajitoe kwamba watajitahidi wawezavyo kuleta maendeleo katika maeneo hayo ;si kitu kundi hata liwe dogo namna gani.Pia ni kwasababu hii ndio maana kundi linaunganishwa ,kiongozi wa kila eneo lililolengwa ni lazima afahamike.

Kwa kadri makundi yanavyokua yatawapanga wanachama wao kwa kadri ya karama,vipawa na mivuto katika moja ya timu tatu. Kila timu italizingatia eneo mojawapo kati ya hayo yaliyotajwa kwa kadri timu zinavyokuwa baadaye zaweza kugawanyika katika timu ndogo ndogo.

Ni muhimu kwamba makundi hayabadili mtindo wake. Mipango mingi ya timu ya Epworth ofisi kuu imekuwa na misingi ya kufikiria kwamba; kwa makadirio ya chini makundi yametoa msaada kwa maeneo haya matatu. Haya maeneo matatu yaliyolengwa yatatumika kwa kuweka mipango ya kazi za timu ya Epworth kama shughuli za Timu ya Epworth,,mipango ya kutoa mafunzo chuoni na tuvuti ya ulimwengu.

Makundi yaliyosajiliwa

Ni makundi ya vijana yaliyowateua viongozi watatu wa timu yana kanisa linalowezeshwa nje ya dhehebu la Epworth United Methodist . Makundi yaliyosajiliwa ni lazima yatume kadi za mkataba ambazo zimesainiwa na viongozi watatu wa kundi lililosajiliwa

Makundi yanayo jiandaa kwanza

Endapo watu wapatao chini ya watatu wanataka kulianzisha kundi ,wanaweza kusajiliwa na ofisi kuu ya timu ya Epworth na kutambulikana kama ni kundi linalotaka kuanza, masharti yanayohusu kundi linaloanza ni haya;

- Viongozi wamesaini mkataba wa Timu ya Epworth .
- Wamelitaja kanisa la kuliwezesha na wamejadiliana juu ya mipango yao na mchungaji.
- Endapo hati A yenye Baraza la Ad linaposaini mkataba wa kanisa au (B) mchungaji ameituma barua pepe kwa ofisi kuu ya Timu ya Epworth ataonyesha kwamba ataliwezesha kundi linaloanza (angalia nyuma ya kitabu hiki).
- Makundi yanayoanza yatawekwa kwenye orodha ya tuvuti ya Timu ya Epworth na msaada utatolewa na kuyasaidia ili yakue.

Ukuzi wa kiroho ni jiwe la pembeni la Timu ya kundi la Epworth . Toka mwanzoni ,timu ya Epworth , kimsingi mtazamo wa timu umekuwa ukilenga juu ya kuwatafuta watu waliopotea na kuwafanya wampate yesu kristo na kuyajenga mahusiano naye.

Maeneo yote yaliyolengwa na yaliyopangwa hapa chini ni lazima yawezeshwe kusudi kila eneo lielekeze kila shughuli kwenye makusudi hayo

1. Maombi

- Maombi ya mkesha na faragha.
- Maombezi na maombi ya mnyororo
- Timu za maombi .

2.Kuabudu

- Panga ibada za tofauti za kila mara.
- Pangilia matukio maalumu ya maombi
- Safari kwa ajili ya matukio

3.Masomo ya Biblia

- Makundi madogo ya kujifunza biblia au makundi ya kujadiliana
- Safari za mikutano ikiwamo ile ya Timu ya Epworth

4.Uinjilisti

- Kwa jamii kwa kupitia mipango mengineyo ya kuwapelekea injili kama vile ile ya timu za mbegu ya Epworth ambayo inayo maua ya kuzaa watu wanaopatikana ghafla ndani ya jamii.
- Katika eneo la nchi na ulimwengu kwa njia ya safari za misheni.

5.Faragha

Yawezekana faragha ikawa ya siku moja au zaidi na ikawa inaunganisha na jambo mojawapo ya hayo yaliyopo hapo juu.
Ofisi kuu ya Epworth itakuwa ikitoa gharama ndogo ,faragha ndefu za juma kwa kupitia mashirika yaliyo na ubia nayo kama vile huduma za "Mission Beles'

Habari zaidi juu ya hizi faragha zitakazotolewa kwenye kundi letu "Face book'
Na www.opworthi eaque . org

6.Mikutano ya timu ya Epworth

Kupanga utaratibu wa kila mara wa kipindi cha mikutano ya Epworth ndani ya wajibu wa timu ya ukuzi wa kiroho ndani ya kundi ambalo limekomaa ,mikutano itahusika na maombi ,kujifunza Biblia na kuabudu.Makundi yanapoanza kujitokeza, mikutano itaanza kuwa ya aina ya ushirikiano,kuabudu na kujifunza Biblia kunaweza kuongezwa.

Imependekezwa kwamba hatimaye kutana mara mbili kwa mwezi kwa dakika 90-120. Majuma mengine yawe ya muda uliopangwa kwa kuijenga walao jumuiya moja na shughuli moja ya kimisheni kwa mwezi.
Mapendekezo ya mikutano ya timu yakiwa na vidokezo;

- Muda wa kusalimiana kabla ya mkutano kuanza
(Kuandaa beji za majina).
- Matangazo.
- Kichekesho(kitu cha kuwafanyia watu wafurahi)
- Nyimbo za kuabudu
-
- Viunganisho na umisheni-Nafasi za umisheni kwa kifupi
- Kizifuatilia changamoto zilizopita
- Wakati wa kufundisha Biblia

- Kuingia katika makundi madogo kwa ajili ya maombi na majadiliano.
- Changamoto zinazotokana na ulimwengu.
- Wimbo na maombi ya kufunga
- Tukio la mahusiano(social event)baada ya mkutano

Timu ya Epworth ya ulimwengu itakuwa inaanzisha ubia wa kusaidia kazi zinazo wezesha kukuwa kiroho.Haya mashirika yatatoa nafasi za utendaji ,na kuelimisha n.k. Makundi yatapata vifaa na mawasiliano kupitia tuvuti ya Epworth ili kurahisisha hatua ya ubia na mashirika haya.

Kwa sasa shirika moja tayari lipo na huduma za "Mission Bells' iliyopo Wisconsin ni kampuni isofanya kazi kwa faida ambayo inasaidia miradi midogo ya kimisheni yenye gharama ya chini na kuiwezesha mikutano ya maombi ya faragha kwa vijana wa wazazi vijana.

Timu za kuijenga jumuiya
Kwa muhitasari;
Timu ya kuijenga jamii inalenga juu ya uhusiano kati ya vijana katika kundi.Maeneo matatu yanayo kusudiwa yatapaswa kusaidiwa .Kazi maalumu zilizopendekezwa katika maeneo hayo yametolewa mapendekezo kama ni mwongozo.

Matukio ya utendaji
Matukio haya hayawaleti washiriki wawe pamoja tu bali yanarahisiasha makundi yawahusishe marafiki zao wawajibike.mifano inahusisha matukio ya michezo,sinema za nyumbani BBQs,kuliwezesha tamasha (uimbaji).kuzileta sinema kanisani, n.k

Matukio.
Matukio yanafanana na faragha lakini yanaweza kuwa na mpangilio ulio na upungufu kidogo wa muda wa kuabudu na kujifunza biblia .Matukio yanakuwa mengi kwa siku ambako wanaoshiriki wanakuwa pamoja kwa muda mrefu wakiyaimarisha mahusiano miongoni mwa watu walio hudhuria .

Kuyajenga mahusiano.
Timu ya kuijenga jamii inayo wajibu wa kufanya kazi na Timu ya misheni ili kuthibitisha kwamba matukio ya timu ya Epworth yanatoa nafasi kujenga mahusiano yenye nguvu ya miongoni mwa washiriki.

Kazi ya kundi la Epworth
Timu ya misheni inatakiwa iwapate wanachama wa kundi husika wa huduma kwa wenye mahitaji.
Timu itapaswa ilenge kwenye maeneo matatu.
Eneo la mahali ,la kitaifa na la kiulimwengu .

Baadhi ya mifano ya kwa kila eneo imetolewa hapo chini.
Makundi yametiwa changamoto njia ya kutofautisha na kutoa ripoti kwenye makao makuu ili yashirikishwe na makundi mengine. Mara tuvuti mpya itakapokuwa tayari,makundi yataweza kuyatuma mawazo yao na kuyashuhudia yale waliyo fanikiwa.

Misheni za mahali.

Timu ya Epworth ina lengo la pekee linalozingatia sana juu ya misheni za mahali.Tunafikiri juu ya hili katika maeneo ya huduma kwa jamii,
Kuliko kutoa huduma ya muda mfupi kwenye mateso ya jamii fulani, Timu ya Epworth inalenga kuliondoa tatizo linaloleta adha au maumivu.Kama lilivyodokezwa hapo awali,kazi ya timu ya Epworth kwa sasa inashughulika na mipango ya ajira na msaada wa mipango ya malezi ili iweze kufanyika kwa kawaida. Mipango hii imelenga kwenye vyanzo kwa jamii nyingi,familia na mambo ya mtu binafsi.

Mambo mengine ya kazi za za misheni ya mahali .

- Kuwatembelea wasio tambulikana na jamii.
- Miradi ya huduma kwa jamii(chakula ,supu jikoni,vilabu vya wavulana na wasichana n.k.
- Huduma ya jamii usiku kutoa chakula cha jioni bure kwa watu kwa kadri mafunzo yanayo anzishwa ulimwenguni na kuwa na mipango ya misheni ya mahali ,hii mipango yaweza kuwa kundi jingine la mradi misheni wan chi au wa ulimwengu. Endapo kundi lenu litahitaji msaada wa mradi wa mahali, tafadhali tuletee taarifa kwa ofisi kuu.Tunaweza kusaidia kuuinua . hatimaye kutakuwapo na picha kwenye tuvuti kubwa kwa ajili ya kupeleka kwenye nafasi za misheni.

Kazi za umisheni ulimwenguni.

- Kuliwezesha kundi lingine juu ya misheni ya mahali kwa kazi au fedha.
- Kuwaendea na injili
- injili (UUPGS) 649 makundi ambayo hayajapelekewa

Leo kuna makundi 632 ambao bado hayajapelekewa injili yenye wakazi zaidi ya 50,000 ambao wangali hawajapelekewa injili ya yesu kristo.Hawa watu 366,000,000 wamepotea kiroho na hawana msaada kama kondoo wasio na mchungaji .Miongoni mwao kristo bado hajafahamika,wala hayajasujudiwa .

Haya makundi 632 pengine ndio wahitaji wa mahitaji.Hawajapatikana katika makanisa maana yake hakuna hata kanisa moja ,hakuna hata shirika moja la kimisheni.hakuna ambaye ameshughulika nao katika kuwaambia juu ya mungu wetu aliye mkuu na mwokozi ,Bwana yesu kristo .makundi yale 632 yapo kwenye kiini kikubwa cha kazi ya agizo lile kuu (mt.28;19-20)kutoka kamati ya kuimaliza kazi(habari zaidi itapatikana kutoka tuvuti ya kundi la Epworth hivi karibuni.

Mweka hazina.
Mwanzoni kundi halitaona zaidi kama kumtumia sana mweka hazina, ingawaje kwa kadri kundi litakapokuwa,wajibu wa kazi ya mweka hazina itaongezeka,

- Kufanya kazi pamoja na mweka hazina wa kanisa kwa kutunza hesabu kwa ajili ya matukio na shughuli mbalimbali .
- Kukusanya misaada
- Kulipia gharama za kundi.
- Kutoa taarifa za pesa kwa timu ya uongozi wa kundi.

Katibu

Baadhi ya kazi za katibu zimeonyeshwa hapo chini.

- Mawasiliano ya kundi
- Kutoa taarifa ya nyongeza kwenye tuvuti kuipeleka kwenye kundi la ulimwengu kwa ajili ya kundi lake.
- Kutoa matangazo kwenye tuvuti magazeti kwenye mbao za matangazo .n.k.
- Kutuma barua – barua pepe kadi za posta,na barua mbalimbali.
- Kuandika miniti za mikutano ya uongozi .
- Kutunza kumbukumbu na kufanya mawasiliano na wote wanaoshiriki.

Kipengele cha Ax; Wajibu wa kanisa linalofadhili
Makundi ya Epworth yanatakiwa yafadhiliwe na kanisa la "United Methodist ; Makanisa mengine yanaweza kuyafadhili makundi mengine yaliyopo chini ya mamlaka yake.)Kulifadhili kundi la timu ya Epworth ni kazi sana.

Kanisa linatazamiwa lilisaidie kundi kwa njia ya maombi,maneno yenye kutia moyo na kutia ushauri pamoja na theologia ya United Methodist kwa ajili ya kundi ili lidumu na kufundisha .

Kufadhili kundi la Epworth halihitaji msaada wowote ule wa kifedha kutokana na kundi isipokuwa wameamua kufanya hivyo.
Wajibu uliomkubwa kwa kundi utakuwa ni kumpa mtu juu ya mchungaji au mlei mkubwa awe `mshauri na kulipatia ushauri kundi.Viongozi wa kundi walio na umri wa kati wanaowajibu wa kuliendesha kundi lakini mshauri aliyeteuliwa na kanisa anaowajibu wa kuhakikisha kwamba kundi linabaki na uaminifu kwa maandiko matakatifu pamoja na imani ya kanisa la ' United Methodist ``Mshauri pia anaweza kuwasaida viongozi wa kundi kwenye mambo magumu ya imani ambayo wanaweza kukutana nayo katika maisha yao na yale ya washiriki wa kundi.inawezekana akalazimika mshauri kuhudhuria baadhi ya mikutano au matukio ya kundi hata kama kwa muda mfupi tu .kusudi apate kujua jinsi gani kundi linavyofanya kazi.
Endapo unayo maswali juu ya wajibu wa kanisa linalo tegemeza ,tafadhali wasiliana na ofisi kuu ya Epworth.
Kuichochea na kuidumisha tabia ya kumweka yesu katikati ulimwenguni-kwa watu katika umisheni.kwa njia ya kuijenga jamii umisheni na kukua kiroho.
``````````

Dokezo(3)Kitu gani kingine kije hapa
``````````

Kipengele Bx-Kulisajili kundi

Jina la kundi lako
Anwani ya kundi lako
Anwani ya posta(kama ni tofauti)
Jina la kanisa lenye ufadhili
Anwani ya kanisa lenye ufadhili

Mchungaji au mwanachama mlezi ambaye ni wa kufanya mawasiliano naye ndani ya kanisa lenye ufadhili.
Barua pepe na namba yake ya simu ya mtu huyo
Anwani ya tuvuti ya kundi lako(endapo ipo)
Jina la mmoja wa viongozi wa kundi
Jina la kanisa na mahali lilipo.

Toa majina na anwani ,barua pepe na namba za simu za watu wanaojaza nafasi za kazi zifuatazo
Kiongozi wa timu ya ukuzi wa kiroho.
Kiongozi wa timu ya kuijenga jamii.
Kiongozi wa timu ya umisheni
Rais
Katibu
Mweka hazina
Ni taarifa ipi ya mawasiliano ambayo ungelipenda iorodheshwe ndani ya kitabu cha orodha ya majina ya timu ya Epworth.

Endapo ungependa jambo lolote lionekane katika gazeti la ;Herald ‘ kuhusu kundi lenu tafadhali uandike juu ya yale yanapotokea kwenye kundi lako andika para mfupi.

Kipengele x. C- Huduma ya kijamii.

Sehemu ifuatayo inatoka kwenye kitabu kinachoitwa “The Efficient Epworthian na Dan Brearley Brummitt :ambaye alikuwa muhariri wa gazeti la League s newspaper the Epworth League Henald.Kitabu hiki kilichapishwa mnamo mwaka wa 1922.

(Lengo la huduma ya jamii)ni ukombozi wa jamii’ Ni ukombozi wa jamii ya watu kutokana na ugonjwa, umaskini, kesi na mateso, maendeleo na ukamilifu wa kazi za kibinadamu zinazohusiana na maisha , na ujenzi wa utaratibu wa kijamii ambao ni mji wa mungu hapa duniani.

KUITAMBUA JAMII
Kundi lolote la huduma ya jamii kwa ajili ya mtu binafsi au kundi lazima liwe na msingi wa mahitaji ya jamii ya mahali, kwa hiyo hayo ni lazima yafahamike. Njia pekee ya kuyatambua ni kupata kuifahamu hali ya mahali pale ambayo itaonesha ni eneo lipi la kazi inayopasa ifanyike.

Kabla ya kufanya kazi yoyote ile, pia kundi linapaswa kutambua ni mashirika gani yako kazini ili kuyaondoa mahitaji ya jamii na namna gani ili kwamba juhudi zake zisiweze kutolewa mara mbili kwa kazi zilizofanywa na vyama vingine, bali kwa kuongezea tu.
Chati hii yaweza kuandaliwa na kuwekwa kwenye ukuta wa kanisa itakayoonesha mashirika yatakayokuwa yanashughulika na umaskini, ugonjwa au kubaguana au kutatua tatizo lolote lile la raia lenye kuhitaji utendaji wa dharura.

Haipaswi kushauriwa wala kuwa inawezekana kwa upande wa timu ya Epworth kufanya uchunguzi kwa jamii yote hasa hasa kwenye maeneo makubwa hasa kwenye jamii kubwa iliyo na wakazi elfu kumi na chini yake, hata hivyo , ingefaa kupata picha ya jumla ya hali zilivyo, lakini hata katika jambo ambalo vijana kwa asili yanawavutia. Hii itafupisha utafiti na kazi na kuielekeza juhudi kwenye mambo machache.
Kundi lolote laweza kushughulikia kwenye eneo la ufumbuzi na kuziboresha hali za maisha ya vijana wa jamii husika. Hii itahusisha hali ya maisha ya jamii na michezo, hali ya elimu, afya, nyumba na kazi.

KITU AMBACHO KILA KUNDI LINACHOPASWA KUJUA JUU YA JAMII AMBAMO LINAKAA

Utaratibu huu wa maswali utaleta msaada kwa kundi katika kuitambua jamii yake:
Umaskini na kubaguana:

Je ni mashirika gani ya ufadhili yaliyopo?
Je wepesi wake upoje?
Upo ushirikiano wowote kati ya mashirika hayo?

Kadiria kiasi kilichotumika kwa ajili ya msaada kwa mwaka na idadi ya matatizo yaliyotatuliwa.
Je ni msaada gani uliotolewa na makanisa?
Je kuna ushirikiano wowote miongoni mwa idara tofauti za kanisa moja na makanisa mengine, na mashirika mengine yanayotoa msaada?
Je ni mji gani, tarafa au msaada uliotolewa na serikali kwa msaada kwa ajili ya umaskini au ugojwa? Je upo ndani ya jamii? Je una mtu anayekagua kazi hii kuhakikisha kuwa msaada unafika kwa wakati muafaka?

Maisha ya jamii na michezo:

Je ni michezo gani inayotolewa mashuleni makanisani Y.M.C.A n.k?
Je ni burudani zipi zinafanyika kwa ajili ya manufaa ya mtu binafsi?
Tabia ya jumla, yoyote yale yaliyo ya fedheha yenye kuharibu?

Ni vifaa gani vya kuelimisha vijana ambao wanapenda kujiendeleza katika elimu huku wakifanya kazi? Shule za usiku? Madarasa maalumu kwenye Y.M.C.A (Chama cha vijana wakikristo na (Y.W.C.A) chama cha wanawake vijana wa kikristo, kozi za mafundisho? Je vifaa hivi vipo?

Afya na nyumba:

Kiwango cha vifo? Vifo vya watoto wachanga ukilinganisha na jamii zinazotuzunguka?
Je idara ya afya inazuia magonjwa yenye maambukizi? Je inapata kuieleza jamii kuchukua tahadhari za kinga?

Je ipo sehemu yoyote ya mji inayoishi jamii kwenye maeneo yasiyopata siha (afya) au iliyo na msongamano wa majumba?

Je ni sheria gani zinazohusiana na hali na je zinatendaje kazi?

Kazi: ni vijana wangapi wa umri zaidi ya miaka kumi na sita wenye kufanya vibarua katika jamii. Ni wangapi kama wapo walio chini ya miaka kumi na sita? Wanafanyia kazi wapi? Ni wangapi wanaofanya kazi zaidi ya masaa kumi? Zaidi ya masaa tisa? Wangapi wanaofanya kazi jumapili?
Je ni wasichana wangapi jumapili wanaofanya kazi usiku?
Je ni kiwango gani cha chini wanacholipwa? Vijana wa kike? Je kuna sheria ya nchi inayosema ni kiwango gani cha chini, je sheria hiyo inatumika?
Wastani wa malipo yanayotolewa viwandani katika jamii hiyo? Je inalinganaje na gharama ya maisha katika sehemu ile?

Je masharti ya afya katika jamii ya viwandani? Je ni sheria zipi za kazi ndani ya nchi? Je hizo sheria zinamlinda mfanyakazi na kwa kiasi gani? Je kuna utaratibu wa ukaguzi viwandani na inatekelezwa?
Je ni jambo gani linalofanyika katika kuwasaidia vijana juu ya kuipata ajira?

Serikali: Ni aina gani ya serikali? Nani ambao ni maafisa? Je kazi yao ni ipi na wanayo mamlaka gani waliyonayo? Je ni nguvu zipi wanazozitumia?
Ni idara zipi za serikali za mitaa ambazo zinawasaidia sana jamii.
Je ni ushirikiano gani uliopo kati ya idara hizi na makundi ya kanisa?

JINSI YA KUANZA

Njia bora namna ya kuanza ni idara ya huduma ya jamii kufanya utafiti wa kawaida wa jamii kwa kufuata mpangilio huu, ukiuboresha mpango huo ili uendane na mahitaji ya mahali hapo na kuyaondoa maswali ambayo hayalingani na sehemu hiyo.
Taarifa hii yafaa tena ipangwe kwenye aina ya chati ili kwamba iwakilishwe kwenye kundi lolote katika mtindo wa grafu. Sinema yaweza kutumika vema zaidi katika sehemu hii ya kazi, kutokana na utafiti huu wa kawaida washiriki wanaweza kuichagua hali ile ambayo inaonekana kuwa inahitaji hatua za haraka sana kiutendaji.

Baada ya kufanya hivyo utafiti zaidi wa kina juu ya hali ile ufanyike kabla ya kitu kingine ili kulitatua. tatizo kwa upande wa makundi ya kwenye mji mkubwa, wilayani ni lazima iainishwe na makundi mengine ya vijana ikiwezekana yaorodheshwe kwenye jitihada hiyo.

KUWA NA HURUMA NA KUSAIDIA KULETA UJENZI

Kazi ya kusaidia kwenye maafa

Kazi yenye kuonyesha utendaji wa kundi la Epworth haiwezi kuitwa huduma ya kijamii mpaka itakapoonekana kuwa ni ya ujenzi na yenye kulindwa, pamoja na kupunguza maumivu. Huduma ya jamii haishughuliki na kupunguza maumivu tu, pasipo kufanya utafiti wa vyanzo vya huzuni na kuvitafutia uvumbuzi.

Kanuni halisi ya kazi ya kusaidia ni ushirikiano. Ushirikiano ndani ya kanisa lenyewe, kuona kwamba kundi moja haliigi kazi ya kundi lingine, ushirikiano na makanisa mengine ya dhehebu lilelile na ushirikiano wa mashirika mengine yaliyo nje ya kanisa hasa yakiwa na mikakati iliyo na mpango maalumu kwa kuisaidia jamii.

Kanuni ya pili ni ya muhimu vilevile kunatakiwa kuwe na huduma endelevu.Msaada mdogo hautaleta jambo dogo zuri tu,bali inaweza kuleta madhara.Hata kama ni kazi gani ambayo inaweza kuchaguliwa.,isiachwe tu mpaka ikamilike hadi mwisho wala kusiwe na hitaji jingine juu ya kazi hiyo.ni vema kulichagua tatizo la kudumu na kulipatia kipaumbele kuliko kujaribu kufanya kazi mbalimbali kidogo kidogo.kwa mfano,endapo familia imepewa msaada itahitaji kuisaidiwa hadi wanafamilia wataka poweza kujitunza wenyewe.
Si kwa kutoa kikapu wakati wa shukrani au siku ya krismas na siku zingine za mwaka wanaachwa peke yao.

Karibu kila kundi miongoni mwa washiriki wake mtu mmoja au zaidi kwa vijana wanawake ambao wanauwezo wa kuutumia muda wao mzuri wa kumtembelea na kutoa msaada. Hawa wanapaswa kufundishwa ili wawe wageni marafiki ndani ya jamii,ili kwamba huduma zao ziongozwe na kuelekezwa ili kwamba kwa njia hiyo zitakuwa na thamani mara mbili. Kikundi cha kutoa huduma cha mahali kitawapokea watu wanaojitoa kama hao,kuwasaidia na kuwafundisha.

Makundi ya vijijini yaweza kutoa matunda na maua kwa wagonjwa mjini wakishirikiana na makundi ya kazi ya usafirishaji wa haraka kwa kawaida zitabeba zawadi hizo bila gharama yoyote.

Kazi kwa ajili ya wagonjwa,ikiwa idara ya Huruma na msaada ikifanya kuwa ni shirika lenye kutoa huduma ya kijamii. Isikomee kwenye msaada peke yake.Ni lazima upanue uwanja wake mpaka iangalie kwenye kinga ya ugonjwa na kupambana na utetezi juu ya hatua za afya .
Idara ya afya ya mahali itapendezwa kuwa na msaada wa mtu atakayekuwa anaeneza juu ya mipango ya afya na uangalifu maalumu juu ya mipango yake ya ugonjwa hasa katika kukiuka kanuni za afya na katika kugawa vipeperushi au vijitabu vinavyohusu afya ya jamii,jitihada zake za kuyamaliza makazi yasiyo kamilika na katika juhudi za kudumisha kanuni ya afya ya jamii.

KUSHIRIKISHA IDARA YA JAMII.

Katika kila jumuiya yapo makundi ya vijana ambao hawajaletwa katika mahusiano na vijana kanisani kwenye vyama vya vijana .Kila kundi linapaswa kuwa na jitihada ya kujaribu kuwasiliana na hawa vijana.

Vijana wasio na makazi
Ebu chukua kwa mfano ,idadi ya vijana na wasichana inavyoongezeka mjini ambao wapo mbali na makwao,bila kuwapo na migahawa iliyokuwapo katika mazingira ya makwao na wasipokuwa na ushirikiano usiokamilika katika mazingira yao mapya.

Msaada unaoweza kutolewa unaweza kuwa ni ule wa kuwatafutia mahali pa malazi penye kufaa, na kuwapata hawa wasio na makazi mwaliko wafike kwenye nyumba za wakristo ili jumapili wawepo.,kusudi waupate mguso wa maisha ya nyumbani. Saa ile ya ushirikiano baada ya ibada ambapo vinywaji ambavyo ni vikali kutolewa ,imetumika kama silaha dhidi ya upweke na hatari za muda huo..

Vijana wanaotoka nchi za nje nao ni wakimbizi wake kwa waume .Kama amerika ingewatunza au kuwajali wageni wanaoingia katika idadi hizo kwa ahadi ya uhuru ulio mkubwa , ingekuwa ni kwa vijana wa kimalekani na hasa wale wa makanisa wangeona katika makundi kama haya idadi iliyokubwa sana.

Tuhuma za rangi na chuki binafsi havitakoma hadi vijana watakapokutana uso kwa uso na kujitafutia umoja muhimu wa jamii.
Masomo ya kiingereza na uraia yanapata nafasi nzuri ya kuzoeana ,sasa kunaidadi kubwa ya vitabu vilivyoandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha wageni kwa rahisi bila lugha ya kiufundi ,ili kwamba mtu aliyesoma vizuri kawaida wa Epworth anaweza kuliendesha darasa hilo vizuri.

Masomo ya kiingereza na uraia yanapata nafasi nzuri yakupata kuzoeana. Kwa sasa kuna idadi kubwa ya vitabu vilivyoandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha wageni kwa rahisi bila lugha ya kiufundi, ikiwa kwamba mtu aliyesoma vema kwa kawaida wa Epworth anaweza kuliendesha darasa hilo vizuri
.
Pamoja na mbinu zako za kuupanua wigo wa urafiki nje ya kundi la kanisa ,Jambo muhimu ni kuingia katika mawasiliano na vijana wa mataifa mengineyo ndani ya jamii, kwakua hii itapata kufungua njia kwa ajili ya huduma kubwa kwa kundi la wakimbizi.

Michezo kwa wote –Je kundi lako linao mpango endelevu wa michezo au hua linatoa nafasi kwa ‘ ushirikiano’ kwa nadra ?Mpangilio ulioandaliwa vizuri unaochukua majira ya nusu mwaka utaleta matunda ya mafanikio kuliko juhudi ya ovyo ovyo tu kuikamilisha michezo. .Mipango inapaswa kupanuliwa ikilihusisha kila kundi linalopatikana ndani ya jamii.Majira yale ya miti kupukutisha majani , mipango yaweza kuanza na karibu ya kawaida, mapokezi ya makundi mbalimbali yaliyokuwa mbali wakati wa kipindi cha joto- walimu, wanafunzi n.k. na mpango utakaokuwa na majira haya waweza kuwa wa aina nyingi kama muziki na jioni za kawaida tu.

Elimu hasa mjini yaweza ikachanganywa kwa pamoja na michezo kwa kutembelea kwa makundi sehemu mbalimbali zenye mvuto mjini .Huu ni mpango mzuri hasa kiangazi jumapili

mchana ,wakati matembezi yanapoishia kwenye maakuli au ushirikiano wa aina ya nje wala sio nyumbani (picnic).